

## **MAANDALIZI YA KUWAPOKEA WANAFUNZI WA KIDATO CHA KWANZA 2018**

Halmashauri ya Manispaa Mtwara – Mikindani imepokea wanafunzi wa kidato kwanza mwaka 2018 wapatao 1,555 wakiwemo wavulana 733 na wasichana 822, ambao kwa ujumla wao watahitaji vyumba vyumbu ya madarasa 39. Jedwali lifuatalo linaonyesha mahitaji ya vyumba vyumbu ya madarasa:-

### **Jedwali Na.1: VYUMBA VYA MADARASA KIDATO CHA KWANZA 2018**

MAHITAJI	YALIYOPO	UPUNGUFU
39	36	3

### **Jedwali Na. 2: HATUA ZA UTEKELEZAJI WA UJENZI WA MADARASA**

NA	JINA LA SHULE	IDADI YA VYUMBA HITAJIKA	HATUA ZA UTEKELEZAJI	MAELEZO
1	Mangamba sekondari	2	Vikao vya maandalizi vya wadau vimfanyika	Ujenzi haujaanza
2	Mitengo sekondari	1	Vikao vya maandalizi vya wadau vimfanyika	Ujenzi haujaanza

Halmashauri imetenga na kipeleka fedha kiasi cha **Tshs. 30,000,000/=** katika shule hizo ili kutekeleza ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa (wastani wa **Tshs. 10,000,000/=** kwa kila chumba). Aidha Halmashauri itatumia benki ya matofari zilizopo katika kata husika na kuendelea kuhamasisha jamii kuchangia nguvu kazi katika ujenzi huo. Taratibu za ujenzi zimeanza na unatarajiwaa kukamilika ifikapo mwezi Februari, 2018.

Halmashauri itafanya ukarabati wa vyumba 02 vya madarasa katika shule ya sekondari ya Naliendele ili kuweza kuwapokea wanafunzi wa kidato cha kwanza. Wakati taratibu za ujenzi zinaendelea wanafunzi wa kidato cha kwanza watasomea katika vyumba vya maabara kwa muda.

Pia, Halmashauri imetenga fedha **Tshs. 6,500,000/=** kwa ajili ya kutengeneza viti 200 na meza 200 ili kila mwanafunzi apate meza na kitu. Taratibu za utengenezaji zimeanza katika shule ya sekondari ya Ufundu Mtwara.

Aidha kwa sasa Halamshauri inafanya ukarabati wa viti na meza shulenii kwa kutumia fedha za ukarabati zilizopo shulenii ambapo wakuu wa shule wanasimamia zoezi hilo kila mmoja katika shule yake.

#### **Jedwali Na. 3: UPUNGUFU WA SAMANI.**

NA.	SHULE	MEZA	VITI
1.	Naliendele Sekondari	58	70
2.	Shangani Sekondari	54	62
3.	Saba Saba Sekondari	88	68
<b>Jumla</b>		<b>200</b>	<b>200</b>

Kwa upande wa matundu ya vyoo Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani ina mahitaji na mapungufu kama ifuatavyo:-

#### **Jedwali Na. 4: MAHITAJI YA VYOO.**

MAHITAJI	VILIVYOPO	UPUNGUFU
258	253	5

#### **Jedwali Na. 5: MAHITAJI YA VYOO KISHULE.**

NA.	SHULE	IDADI YA MATUNDU
1.	Mangamba Sekondari	1
2.	Mitengo Sekondari	1
3.	Saba Saba Sekondari	1
4	Sino Sekondari	2
<b>Jumla</b>		<b>5</b>

Halmashauri imejipanga kumaliza tatizo la vyoo katika shule za sekondari kwa kushirikisha jamii na kutumia benki za matofari zilizopo katika kila kata.

#### **UTOAJI WA CHAKULA CHA MCHANA SHULENI**

Halmashauri ya Manispaa Mtwara Mikindani inaendelea kutoa chakula cha mchana katika shule zake zote za sekondari na za msingi. Kwa mwaka 2017 mwezi Julai Halmashauri ilinunua mahindi gunia 200 na kugawa katika shule zote za serikali ambapo kila shule ilipata gunia za mahindi (kg 100) kati ya 3 hadi 5 kutegemeana na ukubwa wa shule.

Kwa mwaka 2018 Halmashauri imejipanga kusimamia utoaji wa chakula shulenii kwa kutumia sheria ya haki ya mtoto ya mwaka 2009. Wakuu wa shule na walimu wakuu wamewajulisha wazazi na walezi wa wanafunzi jukumu lao la kisheria la kutoa chakula kwa watoto wao wawapo shulenii, nyumbani na mahali pengine Katika vikao vilivyofanyika wakati wa kufunga shule na Vikao vya Bodi na Kamati za shule.

Aidha Halmashauri kwa kutumia Waratibu Elimu Kata, Maafisa Watendaji Kata itaendelea kufafanua dhana ya elimu bila malipo kama inavyoelezwa katika waraka wa elimu na. 6 wa mwaka 2015 kuhusu utekelezaji wa elimu msingi bila malipo, kipengele cha 3.6 wajibu wa wazazi/walezi na kipengele na. 3.7, kwa kuwakumbusha wazazi na walezi wajibu wao wa msingi kwa watoto wao, ambapo kila mzazi anawajibika kumpatia mtoto wake mahitaji ya msingi ikiwemo chakula, sare za shule na vifaa vya kuandikia.

Mzazi atakayekwenda kinyume na sheria hii hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

### **MAANDALIZI YA MITIHANI YA KIDATO CHA PILI, NNE NA SITA 2018**

Halmashauri ya Manispaa Mtwara Mikindani inatarajia kuendesha mitihani ya kitaifa ya kidato cha Pili, Nne na Sita kati ya mwezi Mei na Novemba mwaka 2018. Maandalizi ya mitihani hiyo yameanza kwa usajili wa watahiniwa wa kidato cha sita mwaka 2018. Kama itakavyoonekena katika jedwali hapo chini.

Pia maandalizi ya usajili wa kidato cha pili na cha nne 2018 yanaendelea na usajili huo utaanza mapema Januari 2018 kwa kuzingatia miongozo ya Baraza la Mitihani la Taifa.

**Jedwali Na. 6: WATAHINIWA KWA MWAKA 2018.**

NA	KIDATO	MWAKA WA UDAHILI	IDADI YA WANAFUNZI WAKATI WA UDAHILI			IDADI YA WATAHINIWA		
			WAV	WAS	JML	WAV	WAS	JML
1	Kidato cha II	2017	696	701	1397	1023	1159	2182
2	Kidato cha IV	2015	586	587	1173	726	870	1596
3	Kidato cha VI	2016	96	245	341	287	262	549
<b>JUMLA</b>			<b>1378</b>	<b>903</b>	<b>2281</b>	<b>2036</b>	<b>2291</b>	<b>4327</b>

Aidha ili kuepusha mdondoko wa watahiniwa usio wa lazima Halmashauri imeweka msisitizo katika:-

1. Kudhibiti utoro kwa kukagua mahudhurio na kuchukua hatu za kisheria dhidi ya watoto watoro kwa kuwatumia polisi kata na Afisa mtendaji wa kata husika.
2. Utoaji wa chakula cha mchana shulen, ambapo kila mzazi / mlezi ametakiwa kuchangia chakula cha mtoto wake awapo shulen.
3. Kusimamia ujifunzaji na ufundishaji unaozingatia ukamilishaji wa mihtasari ya masomo ifikapo Mwezi Juni 2018

Kusimamia utoaji wa mitihani na mazoezi ya upimaji ya mara kwa mara na kufanya masahihisho yenye viwango